
# Mwelekeo wa Msimu wa Mvua kwa Ngazi ya Mkoa na Wilaya zake

**MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2023 KWA MAENEO YA KASKAZINI MWA MKOA WA KIGOMA**
**Umetolewa: 24/08/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2023; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa




Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2023 kwa maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali za maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

- (i) *Msimu huu unatarajiwa kutawaliwa na hali ya El Nino ambayo inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika mwenendo wa mvua za msimu wa Vuli, 2023.*
- (ii) *Kwa ujumla mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.*
- (iii) *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.*
- (iv) *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2024.*
- (v) *Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli.*

**Mvua za msimu wa Vuli, 2023**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

***Angalizo:***

*Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani.*

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727N – 00/2023*

(II) Ngazi ya Wilaya

**MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2023 KWA WILAYA YA KAKONKO**
**Umetolewa: 24/08/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kakonko.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023 kwa wilaya ya Kakonko, Kigoma.

**Dondoo muhimu**

(i) *Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kakonko.*

*(ii) Mvua zitaanza wiki ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.*

(iii) *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2024.*

*(iv) Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.*

## Mvua za msimu wa Vuli, 2023 kwa wilaya ya Kakonko

**Zitaanza:** Wiki ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.

**Zitaisha:** Mwezi Januari, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kakonko ni kati ya milimita 380 hadi 400.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2023.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2023.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa nyingi na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

(i). Wadudu waharibifu na mlipuko wa magonjwa ya mifugo na mazao yanayoambatana na mvua nyingi yanaweza kujitokeza.

(ii). Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri mazao pamoja na miundombinu ya kilimo.

(iii). Upatikanaji wa chakula cha Samaki na malisho ya mifugo unatarajiwa kuongezeka.

### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.

(ii). Matumizi sahihi ya mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, vinashauriwa.

(iii). Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.

(iv). Wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz


**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

727N – 00/2023

(II) Ngazi ya Wilaya

**MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2023 KWA WILAYA YA KIBONDO**
**Umetolewa: 24/08/2023**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2023; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kibondo.




Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023 kwa wilaya ya Kibondo, Kigoma.

**Dondoo muhimu**

(i) *Mvua za juu ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kibondo.*
(ii) *Mvua zitaanza wiki ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.*
(iii) *Mvua zinatarajiwa kuisha Januari, 2024.*
(iv) *Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.*

## Mvua za msimu wa Vuli, 2023 kwa wilaya ya Kibondo

**Zitaanza:** Wiki ya pili ya mwezi Oktoba, 2023.

**Zitaisha:** Mwezi Januari, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba-Disemba kwa wilaya ya Kibondo ni kati ya milimita 380 hadi 410.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2023.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2023.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa nyingi na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

(i) Wadudu waharibifu na mlipuko wa magonjwa ya mifugo na mazao yanayoambatana na mvua nyingi yanaweza kujitokeza.
(ii) Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri mazao pamoja na miundombinu ya kilimo.
(iii) Upatikanaji wa chakula cha Samaki na malisho ya mifugo unatarajiwa kuongezeka.

### Ushauri

(i) Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.
(ii) Matumizi sahihi ya mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, vinashauriwa.
(iii) Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.
(iv) Wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Chuo kikuu cha Dodoma, Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

727N – 00/2023